Usuli:
Wakulima wadogo na mtungo wa ugavi

2.1 Kufasili maana ya wakulima wadogo 13

2.2 Mifano ya mitungo ya ugavi unaohusu wakulima wadogo 14

2.3 Vipaumbele na matatizo ya wakulima wadogo 16

2.4 Matatizoya wakulima wadogo/wafanyi kazi 16

KUBEBA CHAI, KITABU CHA PICHA, PICHA NA. 51

Usuli: Wakulima wadogo na mtungo wa ugavi

Katika idadi kubwa ya nchi zinazoendelea, mengi ya mashamba ni yale madogomadogo, na yanakuza mazao kwa ajili ya masoko ya nje. Bidhaa muhimu kama vile kahawa hukuzwa na wakulima wadogo kwa wingi. Hata hivyo, fasili ya mkulima mdogo hutegemea zao na muktadha wa kijamii, kitamaduni, kiuchumi na kisiasa. Vivyo hivyo, kuna aina tofautitofauti za mistano ya jinsi ambavyo wakulima wadogo wanavyofungamanishwa na mitungo ya ugavi na masoko yaliyo juu yao. Sura hii inalenga kufumbua mambo ambayo ni magumu kueleweka na wakulima wadogo katika mtungo wa ugavi. Pia sura hii itaeleza kinaga ubaga masuala muhimu ya kikazi kama wanavyoyaona wakulima wadogo.

2.1 Kufasili maana ya wakulima wadogo

Kwa kawaida fasili hutegemea ukubwa wa shamba. Kwa mfano, serikali ya Kenya inachukulia wazalishaji wadogo wa chai kuwa wale walio na mashamba yenye ukubwa usiozidi hekta 20. Katika nchi nyingine, kama vile Indonesia, shamba la hecta 15 huchukuliwa kuwa shamba kubwa kiasi. Tapo la biashara isiyopendelea hutumia utegemezi wa kazi ya wanafamilia kama msingi wa fasili yao. Hata hivyo tunaweza kuona kwamba wakulima wadogo:

- Huzalisha kiasi kidogo cha mazao katika ploti ndogo za ardhi,
- Wanaweza kuzalisha bidhaa za kuuza katika masoko ya nje kama shughuli yao kuu ya kujikimu maishani au kama mojawapo ya shughuli zao za kujikimu maishani;
- Kwa jumla, wana vifaa vichache kuliko wakulima wakubwa;
- Kwa kawaida, huchukuliwa kuwa sehemu ya uchumi isiyo rasmi (huenda wasitambuliwe na serikali, huelekea kutengwa katika mambo ya utungaji sheria za kazi, wana kumbukumbu chache za kimaandishi;
- Wanaweza kuwa ni wanaume au wanawake;
- Wanaweza kutegemea familia zao kufanya kazi; lakini pia wanaweza kukodi
- Idadi kubwa ya wafanya kazi;
- Mara kwa mara hudhulumiwa katika mitungo ya ugavi

Tafiti mbili zifuatazo, kutoka Kenya, zinaonyesha sifa maalum za wakulima wadogo

Mkulima mdogo wa mazao mabichi nchini Kenya.

Joseph Kimiti (jina limebadilishwa ili kuweka siri) ni mkulima wa kiume mwenye umri wa miaka 34. Amesoma hadi shule ya upili na hukuza maharagwe ya kifaransa katika eneo la ekari 0.5 la shamba lake la ekari 3 huko wilayani Kirinyaga mkoa wa Kati? Mashariki?? nchini Kenya. Ana mke na watoto wawili wenye umri wa miaka minane na mitano. Watoto hao ni wanafunzi. Mbali na maharagwe ya kifaransa, yeye pia hukuza kahawa na nyanya kama mazao ya biashara. Vilevile, ametenga ekari 0.25 kukuzia vyakula vya nyumbani. Kimiti na mkewe hufanya kazi shambani na pia huajiri vibarua sita (wa kiume na kike) wenye umri wa kati ya miaka 18 hadi 20. Shamba lao liko umbali wa kilomita tano kutoka kituo kinachonunuliwa bidhaa zao. Maharagwe haya husafirishwa huko kwa baiskeli. Hata hivyo, wakati wa mvua Kimiti hupata matatizo ya kupeleka mazao yake katika kituo hicho kwa baiskeli mapema. Kwa sababu hiyo ubora wa zao unaathirika na kiasi kikubwa chake kukataliwa jambo lisababishalo kupunguka kwa mapato yake.

Hata hivyo, Joseph Kimiti, ambaye amekuwa akiuza maharagwe ya kifaransa kwa mmojawapo wa wazalishaji wakubwa zaidi nchini Kenya wa matunda na mboga kwa muda wa miaka mine, anasema kuwa mapato kutokana na mazao mabichi yamemsaidia kuboresha mapato ya familia yake. Ameweza kujenga nyumba ya kudumu (ya mawe) akitumia mapato kutokana na maharagwe hayo.

Mkulima mdogo wa chai nchini Kenya

Kenneth Ngetich (jina limebadilishwa ili kuweka siri) ni mkulima wa kiume mwenye umri wa miaka 45 aliyesoma hadi shule ya msingi. Yeye hukuza chai katika ploti ya ekari 2 wilayani Kericho mkoa wa Bonde la Ufa nchini Kenya. Mbali na chai, yeye pia hukuza mahindi na maharagwe mekundu kama mazao ya biashara katika shamba lake la ekari 6, ambapo ekari 0.5 pekee ndiyo hutumika kukuza vyakula vya nyumbani. Ingawa Kenneth Ngetich hutegemea sana amilia yake kumsaidia kufanya kazi ya shamba, ameajiri mfanyakazi mmoja wa kiume. Nyakati za mazao mengi zaidi, huwa mara kwa mara anaajiri vibarua wa kike (wenye umri kati ya miaka 20 30) kuvuna chai.

Kenneth Ngetich amekuwa akiuza chai kwa mojawapo ya kampuni kubwa za chai nchini Kenya kwa muda wa miaka 12. Anasema kuwa ingawa mapato hayo yamekuwa yakididimia miaka ya hivi karibuni, ameweza kuelimisha wanawe na mapato hayo. Anasema kuwa yeye hupata malipo ya ziada wakati ufaao ambapo shule hufunguliwa muhula wa kwanza[1]. Ingawa shamba lake liko umbali wa kilomita moja tu kutoka kunakonunuliwa chai, Kenneth Ngetich analalamikia uchelewe haji wa mara kwa mara katika kituo hicho, ambao huathiri vibaya ubora wa chai na kupunguza mapato yake. Aidha anaonyesa kuwa bei anayopewa si sawa ikilinganishwa na wakati.

Wakulima wadogo wanaweza pia kuitwa wakulima wa kandokando. Istilahi hii 'mkulima wa kandokando' hutumiwa kwa kawaida kumaanisha wakulima wadogo walio na ushirika ulio rasmi zaidi na muuzaji bidhaa katika soko la nje. Hata hivyo, istilahi hizi mbili hutumiwa kwa njia tofauti ulimwenguni katika miktadha tofautitofauti. Katika kitabu hiki tumetumia istilahi ya mkulima mdogo kumaanisha istilahi zote mbili.

2.2 Mifano ya mitungo ya ugavi inayohusu wakulima wadogo

Wakulima wadogo wanaonekana kuwepo katika mifano anuwai ya mtungo wa ugavi. Wanaweza kuuzia mfanya biashara wa soko la nje au chama cha ushirika moja kwa moja, ama shamba jingine kupitia kwa mfanya biashara mwingine au kupitia mnada. Njia hizi tofautitofauti zitaathiri hali ya mkulima mdogo, pamoja na faida na matatizo yanayowakumba. Kuna madaraja mengi zaidi kati ya wanunuzi wa moja kwa moja na muuzaji wa rejareja, ikiwa ni pamoja na wafungaji mazao kwenye vifurushi, maajenti na wagawaji. Kielelezo kinachofuata kinaonyesha aina mbalimbali za mitungo ya ugavi inayohusisha wakulima wadogo na njia mbalimbali ambazo wanaweza kufungamanishwa nazo.

1. Wakulima wadogo wanalipwa mwishoni mwa mwezi baada ya kupeleka majani chai (malipo ya kwanza). Malipo ya ziada ya chai (malipo ya pili) hulipwa kila mwaka wa kupeleka majani chai; malipo haya hutegemea bei ya chai iliyokuwepo mwaka unaohusika. [mwisho wa tafiti]


Mifano ya mitungo ya ugavi inayohusu wakulima wadogo
Mazao yasiyo haribika kwa haraka
Mazao mabichi
Wauzaji wa reja reja
Wagawaji wa uwingereza
Agenti wa kimataifa
Soko
Watu wa kati
Mashamba makubwa
Wanunuzi wa uwingereza
Makampuni ya kufunga bidhaa katika vifurushi
Vyama vya ushirika
Mashamba
Wakulima wadogo

2.3 Vipaumbele na matatizo ya wakulima wadogo

Utafiti uliofanywa na maulama, wauzaji rejareja na wafanyabiashara wa masoko ya nje unaonyesha kuwa uhusiano kati ya wakulima wadogo na wale wanaonunua kutoka kwao huwa mara kwa mara unakumbwa na ukosefu wa mawasiliano na uwazi. Utafiti wetu wa mitungo ya ugavi wa wanachama unathibitisha tatizo hilo. Ubayana katika mtungo wa ugavi ni muhimu lakini mara nyingi unakosekana. Wakulima wadogo na wafanyakazi wao ni miongoni mwa wale wasiotarajiwa sana kufahamishwa kuhusu mtungo ulio juu yao.

Utafiti uliofanywa, pamoja na ule tulioufanya na wakulima wadogo nchini Kenya katika mradi huu, unaonyesha kuwa wakulima wadogo wanahitaji ya:

- Mikataba iliyoandikwa kati yao na wanunuzi
- Notisi ya mapema ya masharti kuhusu bei, kiasi na sehemu waliyotengewa
- Ubayana zaidi katika kupima au kupanga ubora wa mazao
- Habari zaidi kuhusu masoko, mitungo ya ugavi na kalenda ya uuzaji wa rejareja
- Kufikia wanunuzi kadhaa badala ya kutegemea mnunuzi mmoja
- Kupata vifaa kwa bei nafuu ili kuepuka madeni
- Mafunzo na ushauri zaidi wa kiutendaji kuhusu upanzi wa zao/mazao
- Usaidizi wa maendeleo ya muundo msingi
- Kuimarisha uwezo wao
- Kulipwa vizuri zaidi, kwa wakati mzuri na mara kwa mara (ili waweze kupanga matumizi yao)
- Kundi la kuwakilisha matakwa yao
- Fedha za kununulia vifaa vya kujikinga, mbegu na vivadudi
- Usaidizi wa kuhifadhi kumbukumbu
- Upatikanaji wa mbegu kwa wingi zaidi
- Kupata maji ya kunyunyizia mimea kwa urahisi zaidi

2.4 Migogoro baina ya wakulima wadogo na wafanya kazi

Wafanya kazi walioajiriwa na wakulima wadogo (hata wakulima wenyewe) mara kwa mara hukumbwa na ukosefu wa:

- Maji ya kunywa
- Vyoo vya kutosha
- Mavazi ya kujikinga
- Uhuru wa kushirikiana na wengine
- Kufikia vituo vya kimatibabu
- Ujira
- Malipo ya likizo ya ugonjwa na ya kila mwaka, na ya kazi ya ziada

Wanaweza pia kusumbuliwa

Mwongozo huu unaonyesha jinsi ambavyo washiriki wote katika mtungo wa ugavi, ikiwa ni pamoja na wakulima wadogo wenyewe, wanaweza kuchangia katika kusuluhisha matatizo hayo.